Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili A: literature – Standard level – Paper 1
# Swahili A : littérature – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili A: literatura – Nivel medio – Prueba 1

Wednesday 4 May 2016 (afternoon)
Mercredi 4 mai 2016 (après-midi)
Miércoles 4 de mayo de 2016 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

### Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a guided literary analysis on one passage only. In your answer you must address both of the guiding questions provided.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

### Instructions destinées aux candidats

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez une analyse littéraire dirigée d'un seul des passages. Les deux questions d'orientation fournies doivent être traitées dans votre réponse.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[20 points]**.

### Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un análisis literario guiado sobre un solo pasaje. Debe abordar las dos preguntas de orientación en su respuesta.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.

2216 – 0199

5 pages/páginas

© International Baccalaureate Organization 2016

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi. Ni lazima kuzingatia maswali mawili uliyotolewa kama mwongozo kwenye jibu lako.

**1.**

Bwana Hogo aliyapenda sana maisha ya mji kwa sababu ya anasa zake na mambo kadha wa kadha, kama senema, mipira mikubwamikubwa, yote ambayo yalimfanya akasahau maisha ya shamba. Anasa hizi zilimfanya akaamua akae mjini.

Elimu yake ilikuwa ndogo sana na haikumwezesha kupata kazi ya maana yenye mshahara mzuri wa kumtosha. Ingawa hakuwa na namna ya kuikwepa hiyo hamu yake ya kupenda anasa, ilimbidi atimize vile atakavyo ingawa kwa vyovyote vile maisha yake hayatakuwa mazuri na hawezi kuyaacha.

Hivyo kufuatana na elimu yake, alipata kazi ya mshahara wa kadiri tu usiomwezesha kupata starehe zile azitamanizo; lakini alijigagamiza kwa nguvu ilimradi aambiwe yuko hapo mjini Kimunyu. Mji huu wa Kimunyu ni mji mzuri sana wenye sifa za mambo mengi ya starehe na ni mji wenye amani sana; watu hujifanyia mambo yao bila wasiwasi wowote. Mahoteli makubwa, viwanja vya mipira, majumba ya senema hayaulizwi, ilimradi mambo ya anasa kwa wingi. Bwana Hogo aliona hakuna mji unaoshinda Kimunyu, hivyo mshahara wake aliokuwa akipata ulikuwa kila siku haumtoshi kwa mambo yalivyokuwa mengi na pesa zake kidogo, lakini kama nilivyosema, alijigagamiza.

Aliongeza bidii katika kazi yake na akaongezwa vijipesa kidogo. Alikuwa akipata shilingi mia mbili na hamsini, akafika mia mbili na sabini, lakini nyumba ya kupanga na chakula havikuwa rahisi, hivyo mambo hayo yakimmalizia pesa lakini pia hakujali. Haidhuru siku moja baada ya kupokea mshahara wake tu, alienda akapumzika katika hoteli moja kubwa, halafu akaingia katika taabu zake mpaka mwisho wa mwezi mwingine, akiwa hana akiba yoyote anayojiwekea ili ije imfae baadae. Madeni yalimwandama sana. Mwisho alikuwa hawezi kutembea mchana kama atakavyo ila alitembea kwa dira maana njia nyingine zilikuwa hazimfai kwa sababu ya wadeni wanaomdai. Baada ya kupita muda mrefu wadeni wakaongezeka, naye akawa hodari sana wa kuwakwepa. Yeye alijua kufanya starehe zake tu bila ya kujali haki za watu alizochukua na kutumia kama zake, wala haimjii fikra ya kwamba pesa ya watu ilihitaji kurudishwa na pia alisahau kuwa wale ni watu kama yeye ambao wangeweza kumchukulia hatua ya kisheria.

Baada ya muda, wale wadeni wa Bwana Hogo walikutana kama watatu hivi wakamtafuta kwa umoja na wakampata. Walipomuuliza vipi pesa zao mbona hajawalipa kama alivyoahidi, hakuwa na majibu yenye mwangaza bali aliwapangapanga tu na kutoa ahadi za uwongo maana hakutimiza yote aliyoahidi, na kila mmoja alimpa ahadi yake peke yake; lakini pia wote hakuwatimizia. Lakini kama tujuavyo, njia za mwongo fupi. Hivyo aliposhindwa kutimiza na muda ukapita, wale wadeni walikutana tena wakaamua waende wakamshtaki mahakamani, hakukuwa na njia nyingine ila hiyo. Watu kama watano hivi, walikwenda mahakamani; wengine walimwonea huruma wakamsamehe na kusema atakuja walipa baadaye. Wale walioamua kwenda kumshtaki wakaenda bila ya kuchelewa, wakalipa gharama za mahakama, naye Bwana Hogo mara aliona karatasi za kuitwa kwenye kesi zamwingilia kwa fujo kabisa. Hakugutuka peke yake bali mkuu wake wa kazi pia aliona mambo yaliyomfika Bwana Hogo, si madogo. Alimwita Bwana Hogo ofisini mwake kumwuliza habari zile amweleze kwa kinaganaga maana ni mambo ambayo hajapata kuyaona. “Karatasi tano za kuitwa mahakamani kwa mpigo!” Hapo Bwana Hogo alikuwa hana la kusema isipokuwa jasho chapa lamvuja; hana la kufanya wala la kumwambia mkuu wake wa kazi. Alibaki kubabaika tu na kusema, “Hawa jamaa nilikwisha zungumza nao vizuri sana na tukapatana kuwa nitawalipa lakini tabia zao si nzuri. Hawana ahadi hata kidogo. Unaona mambo waliyoyafanya sasa? Hivi ni vizuri kweli? Na hasa haja yao ni kitu gani hata wakaamua kufanya hivi?” Lakini yeye hakumbuki yale aliyowafanyia ya kuwadanganyadanganya mpaka wakakasirika na wala hayaelezi kamwe.

https://xtremepape.rs/

Anawalaumu tu kwa vile mambo yalivyomharibikia. Wakati huo wote mkuu wake wa kazi amenyamaza kimya anamtazama tu. Yeye akaropoka mpaka mwisho. Mkuu wake wa kazi akawa anamtazama na huku anafikiria la kumwambia maana yalimshangaza sana. Akawa anakariri kimoyomoyo, “Karatasi tano za wadeni kwa pamoja, tena watu mbalimbali, na pesa anazodaiwa ni zaidi ya mshahara wake mara nne; atazilipaje na kwa muda gani! Ni mambo makubwa haya, lakini kabla ya kuamua jambo la kufanya, kwanza ningojee mpaka kesi zitakapokwisha na zitaamuliwaje. Hapo ndipo nitakapojua la kufanya.” Lakini tangu pale awali, moyo wake ulimpiga fundo na mapenzi yake kwa Bwana Hogo yalipungua sana na kumwona ni mtu jambazi mwenye kupenda tabia ya kula haki za watu na bila ya kutekeleza ahadi zake, na si mwaminifu kwa mali ya watu. Alianza kumfikiria vibaya.

Salim A Kibao, *Matatu ya Thamani* (1975)

(a) Hadithi hii inakufundisha nini kuhusu Bwana Hogo na uhusiano wake na wahusika wengine?

(b) Ni mbinu zipi za lugha na kwa njia gani zimetumika kuelewa sifa za Bwana Hogo?



https://xtremepape.rs/

**2.**

**Moyo**

Moyo wanambia imba, dikteta simwimbie, asilani,
Moyo wanambia lumba, muhitaji mlumbie, duniani,
Moyo wanambia chimba, maovu uyachimbue, kifichoni,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia kuwa, ila kasuku usiwe, maishani,
Moyo wanambia iwa, kunguni ila usiwe, shughulini,
Moyo wanambia pewa, cha mnyonge usipewe, chochoroni,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia nenda, penye dhuluma ‘senende, shirikani,
Moyo wanambia penda, mnyonyaji simpende, mlaani,
Moyo wanambia ponda, ateswaye simponde, umwauni,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia, tenda, lenye jamala litende, duniani,
Moyo wanambia unda, lenye faida liunde, kwa insani,
Moyo wanambia tunda, lisilo sumu litunde, la kinywani,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia ota, kuwa mwizi usiote, siwe kaini,
Moyo wanambia kata, mirija yote ikate, mizizini,
Moyo wanambia teta, penye dhuluma patete, andikoni,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia nyosha, penye na kombo panyoshe, pawe laini,
Moyo wanambia usha, mateso yote yaushe, ya pipani,
Moyo wanambia isha, yenye majonzi yaishe, maningani,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia waza, yalopita yawazie, akilini,
Moyo wanambia kaza, mwovu njia mkazie, ‘we kizani,
Moyo wanambia vyaza, lenye heri tuvyazie, petu nchini,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia kosoa, penye ila pakosoe, kwa yakini,
Moyo wanambia ondoa, mawi yote yaondoe, ya jaani,
Moyo wanambia ongoa, penye huzuni wongoe, simanzini,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

Moyo wanambia gombea, lenye haki ligombee, maishani,
Moyo wanambia pepea, ja beramu upepee, duniani,
Moyo wanambia kazia, lenye wema ukazie, maishani,
Moyo wanambia woga, ndio mwanzo wa maafa.

KW Wamitila, *Tamthilia Ya Maisha* (2005)

https://xtremepape.rs/

(a) Jadili mkinzano wa hisia za moyo wa mshairi na maudhui yake katika shairi hili.

(b) Ni kwa njia ipi mshairi ametumia takriri na umuhimu wake ni nini kuwasilisha ujumbe katika shairi?

https://xtremepape.rs/